



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE



Simu Na: +255 (026) 2740016  
Nukushi: +255 026 2740103  
BaruaPepe: ded@makete.go.tz  
Tovuti: http://www.maketedc.go.tz  
*Unapojibu tafadhali taja;*

Kumb. Na.JA.172/302/01/161

Ofisi ya Mkuugenzi Mtendaji,  
Halmashauri Wilaya ya Makete,  
4 Barabara ya Bomani,  
59582 MAKETE, NJOMBE,  
S.L. P 6, MAKETE

29/11/2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA AFISA HESABU DARAJA LA II NAFASI NNE (4)**  
Mkuugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia nafasi nne (4) ya kazi ya Afisa Hesabu Daraja la II wa Mkataba kwa Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

**1. SIFA ZINAZOHITAJIKA**

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe na Shahada ya Kwanza ya Uhasibu, uzoefu kazini wa angalau Miaka 3
- iv. Waombaji wote wawe hawazidi miaka arobaini na tano (45) na hawapungui umri wa miaka kumi na nane (18).
- v. Asiwe na makosa ya jinai

**2. MASHARTI YA AJIRA**

- i. Ajira ya mkataba (miezi sita) "renewable"

**3. NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya Mshahara kwa mwezi ni TGS D

**4. MAJUKUMU YA KAZI YA UHASIBU**

- i. Kutayarisha Makadirio ya Bajeti na kudhibiti matumizi ya fedha pia kuandaa taarifa ya matumizi ya robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima kwa ajili ya kuiwasilisha kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali.
- ii. Kuandaa taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- iii. Kuandaa na kuidhinisha malipo mbalimbali ya shughuli za kila siku za uendeshaji wa ofisi pamoja na shughuli za kutoa huduma kwa wananchi.
- iv. Kufuatia kwa ukaribu matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa matumizi hayo yanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, miongozo ya Programu na Mpango na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika.
- v. Kutayarisha taarifa za hali ya kifedha (financial statements) za programu na kuziandaa kwa ajili ya ukaguzi wa ndani na nje ya taasisi kwa kuzingatia Miongozo ya Serikali na Programu.
- vi. Kuchambua taarifa za kifedha za miradi mbalimbali kwa lengo la kubaini changamoto za utekelezaji na kushauri namna ya kutatua changamoto hizo.